JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# HOTUBA YA WAZIRI WA NCHI OFISI YA RAIS, MAHUSIANO NA URATIBU, MHESHIMIWA STEPHEN MASATO WASIRA (MB), AKIWASILISHA KATIKA KAMATI YA BUNGE ZIMA MAPENDEKEZO YA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA 2015/16

**OFISI YA RAIS, TUME YA MIPANGO**

**NOVEMBA, 2014**

## UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu likae kama Kamati ya Mipango kujadili Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo 2015/16.

2. **Mheshimiwa Spika,** natanguliza shukrani zangu kwako binafsi na waheshimiwa wabunge wote kwa kunipa nafasi ili niweze kuwasilisha Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2015/16. Aidha, napenda kuishukuru kamati ya Bunge ya Bajeti chini ya uenyekiti wake Mheshimiwa Andrew John Chenge Mbunge wa Bariadi Magharibi kwa ushauri muhimu waliotupatia ili kuboresha mapendekezo haya. Naahidi kuwa, Tume ya Mipango itaendelea kuzingatia maoni na mapendekezo yanayotolewa na waheshimiwa wabunge katika hatua mbalimbali za uandaaji na utekelezaji wa mipango ya maendeleo ya Taifa.

3. **Mheshimiwa Spika,** natoa pongezi kwa waheshimiwa wabunge wote chini ya uenyekiti wa Mheshimiwa Samwel John Sitta (Mb) kwa kujadili na hatimaye kufanikisha kupatikana kwa Katiba Mpya inayopendekezwa. Ni matumaini yangu kuwa tutaendelea kushiriki ipasavyo katika hatua zinazofuata katika mchakato wa Katiba Mpya, na hatimaye kuwawezesha Watanzania kupata Katiba Mpya.

4. **Mheshimiwa Spika,** Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2015/16 ni ya mwisho katika mfululizo wa mipango ya kila mwaka ya kutekeleza Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2011/12 – 2015/16). Hivyo, mapendekezo haya yamezingatia vipaumbele vya Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano ambavyo ni: (i) Miundombinu; (ii) Kilimo; (iii) Viwanda vinavyotumia malighafi za ndani na kuongeza thamani; (iv) Maendeleo ya rasilimali watu na ujuzi; na (v) Uendelezaji wa huduma za utalii, biashara na fedha.

5. **Mheshimiwa Spika,** Mapendekezo ya Mpango ninayowasilisha ni mwongozo wa kuandaa miradi na programu za maendeleo zitakazojumuishwa katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2015/16 na kitabu cha bajeti ya maendeleo 2015/16 (Vol. 4). Uandaaji wa miradi na programu kwa mwaka 2015/16 utazingatia miradi ya kitaifa ya kimkakati ikijumuisha ile ya Programu ya Matokeo Makubwa Sasa, na maeneo mengine muhimu kwa ukuaji wa uchumi.

## UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA 2013/14 NA ROBO YA KWANZA YA MWAKA 2014/15

6. **Mheshimiwa Spika**, napenda nieleze kwa muhtasari mapitio ya hali ya uchumi kwa mwaka 2013 na nusu ya kwanza ya mwaka 2014 (Januari – Juni

2014); na utekelezaji wa miradi na programu za maendeleo kwa mwaka 2013/14 na robo ya kwanza ya mwaka 2014/15 kwa baadhi ya miradi.

## Mwenendo wa Uchumi kwa Mwaka 2013 na nusu ya kwanza ya mwaka 2014

7. **Mheshimiwa Spika,** Pato halisi la Taifa kwa mwaka 2013 lilikua kwa asilimia 7.0 ikilinganishwa na asilimia 6.9 mwaka 2012. Katika kipindi cha Januari - Juni 2014 Pato la Taifa lilikua kwa asilimia 7.1 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 7.4 katika kipindi kama hicho mwaka 2013. Katika robo ya kwanza (Januari – Machi, 2014) mfumuko wa bei ulikuwa asilimia 6, na robo ya pili (Aprili – Juni, 2014) asilimia 6.4. Aidha, mfumuko wa bei uliendelea kuongezeka na kufikia asilimia 6.7 Agosti 2014 na kushuka kidogo hadi asilimia 6.6 Septemba 2014. Hii ni kutokana na kupungua kwa mfumuko wa bei za vyakula na vinywaji baridi kutoka asilimia 8.8 Agosti 2014 hadi asilimia 8.5 Septemba 2014.

8. **Mheshimiwa Spika,** Pato la Taifa mwaka 2013 lilikuwa shilingi milioni 53,174,678 kwa bei za mwaka 2013 na idadi ya watu ilikadiriwa kuwa 44,827,757 mwaka 2013. Hivyo, Pato la wastani la kila mtu lilikuwa shilingi 1,186,200 sawa na dola za Kimarekani 706 kwa bei ya mwaka 2013 ikilinganishwa na shilingi 1,025,038 sawa na dola za Kimarekani 600 kwa bei ya

mwaka 2012, ikiwa ni ongezeko la asilimia 15.7. Hivyo, ili kufikia pato la wastani wa dola za Kimarekani 3,000 sawa na shilingi 4,837,184 ambalo ni la uchumi wa kipato cha kati ni dhahiri tunahitaji msukumo zaidi ambao utatuwezesha kufikia kundi la chini la nchi zenye uchumi wa kipato cha kati kuanzia dola za Kimarekani 1,036 hadi 4,085, sawa na takriban shilingi 1,670,032 hadi 6,586,632.

**Mapitio ya Utekelezaji katika Sekta Mbalimbali**

9. **Mheshimiwa Spika,** sasa naomba nieleze kwa kifupi hali ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa mwaka 2013/14 na robo ya kwanza ya mwaka 2014/15 kwa baadhi ya miradi.

10. **Mheshimiwa Spika,** katika eneo la **reli**, mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na: kutandikwa km 89 za reli yenye uzito wa ratili 80 kwa yadi katika eneo la Kitaraka - Malongwe; kukamilika kwa matengenezo ya vichwa nane vya treni na kuanza kutumika; kukamilika kwa ukarabati wa mabehewa 82 kati ya 125 ya mizigo; kukamilisha malipo kwa ajili ya ununuzi wa mabehewa 34 ya breki, mabehewa 274 mapya ya mizigo na 22 mapya ya abiria na kuwasili kwa mabehewa 25 ya kubebea kokoto; kukamilika kutandikwa kwa njia ya reli yenye uzito wa ratili 56.12 kwa yadi katika maeneo yaliyopo stesheni ya Lumbe kuelekea mto Ugalla na maeneo ya stesheni ya mto

Ugalla kuelekea Katumba; kukamilika kwa ujenzi wa madaraja yaliyopo km 293, km 303 na km 517 kutoka Dar es Salaam; kuanza kazi ya usanifu wa kina katika reli ya Tanga Arusha na kukamilika kwa upembuzi yakinifu na usanifu wa awali wa ujenzi wa reli mpya kwa kiwango cha kimataifa *(standard gauge)* kutoka Arusha hadi Musoma; na kukamilika kwa upembuzi wa kina kwa ajili ya uboreshaji wa reli ya Dar es Salaam – Isaka - Kigali.

11. **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa **barabara** mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na:- kukamilika kwa ujenzi wa kilomita 699.15 za barabara kuu kwa kiwango cha lami sawa na asilimia 141 ya lengo la kilomita 495 kwa mwaka 2013/14 na kukamilika kwa ukarabati wa kilomita 233 za barabara kuu kwa kiwango cha lami sawa na asilimia 123 ya lengo la kilomita 190 kwa mwaka 2013/14. Kwa upande wa **madaraja na vivuko**: madaraja ya Nangoo, Maligisu, na Ruhekei yamekamilika; ujenzi wa madaraja mengine upo katika hatua mbalimbali kama ifuatavyo: Sibiti (asilimia 21); Kigamboni (asilimia 60); Kilombero (asilimia 15); Mbutu (asilimia 96) na Kavuu (asilimia 36). Vile vile, ujenzi wa kivuko cha Malagarasi na ukarabati wa vivuko vya MV Chato, MV Kome 1, MV Geita na MV Magogoni umekamilika. Aidha, ujenzi wa kivuko kitakachotoa huduma kati ya Dar es Salaam na Bagamoyo unaendelea huko Bangladesh.

12. **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa **bandari**, hatua iliyofikiwa ni: kukamilika kwa upembuzi yakinifu na kusainiwa kwa makubaliano na Benki ya Dunia ya kuongeza kina gati na 1 hadi 7 pamoja na upanuzi wa njia ya kuingilia katika bandari ya Dar es Salaam; kusainiwa kwa makubaliano ya ujenzi wa bandari ya Bagamoyo; na kutangazwa kwa zabuni kwa ajili ya kupata wawekezaji katika bandari za Mtwara na Mwambani - Tanga.

13. **Mheshimiwa Spika,** katika eneo la **maji safi na majitaka** mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na:- ***mradi wa maji Ruvu Chini***: kukamilika kwa ujenzi wa mtambo wa kusafisha maji na utandazaji wa mabomba kutoka Bagamoyo hadi Dar es Salaam kufikia kilomita 48 kati ya kilomita 55.93 za mradi wote sawa na asilimia 85. Kwa upande wa ***mradi wa maji Ruvu Juu***: mkataba kwa ajili ya ujenzi wa bomba umesainiwa Januari, 2014 na mkandarasi amekamilisha utafiti wa udongo na uchunguzi wa awali wa matanki ya Kibamba na Kimara. Kwa upande wa ***miradi ya maji vijijini***, jumla ya miradi ya maji 489 ilijengwa na kukamilika. Idadi hii inatokana na ujenzi wa miradi 290 ya vijiji 10 katika kila Halmashauri na miradi mingine ya vijiji 199 ya upanuzi na ukarabati iliyotekelezwa chini ya programu hiyo. Miradi hiyo imevipatia maji vijiji 554 na kunufaisha watu 4,975,344. Aidha, jumuiya za watumia maji *(COWSCO's)* 373 zimeundwa na kuanza kutoa

huduma vijijini.

14. **Mheshimiwa Spika,** katika eneo la **nishati**, kazi zilizofanyika ni kama ifuatavyo: ujenzi wa bomba la gesi lenye urefu wa km 542 na kipenyo cha inchi 36 kutoka Mnazi bay (Mtwara) na Songosongo (Lindi) hadi Dar es Salaam umefikia asilimia 88. Vilevile, ujenzi wa bomba la baharini kati ya Songo Songo na Somangafungu lenye urefu wa kilomita 25.6 umekamilika. Kwa upande wa mradi wa umeme Kinyerezi (MW 150), hatua iliyofikiwa ni kufungwa kwa mitambo miwili yenye uwezo wa kuzalisha jumla ya MW 75 na kuwasili kwa mitambo mingine miwili ya uwezo kama huo; ujenzi wa matanki mawili (2) ya kuhifadhia mafuta kwa matumizi ya dharura umefikia asilimia 80; na ujenzi wa majengo ya utawala, karakana na miundombinu ya barabara na maji ndani ya eneo la mradi unaendelea. Aidha, jumla ya wateja 250,340 wapya wameunganishiwa umeme dhidi ya lengo la kuunganisha wateja 193,750 kwa kipindi cha Julai 2013 hadi Septemba 2014; na TANESCO imepunguza upotevu wa umeme kutoka asilimia 21 (2012) hadi asilimia 19 (2014).

15. **Mheshimiwa Spika,** mafanikio yaliyopatikana kwa upande wa miradi ya **umeme vijijini** ni pamoja na: kupeleka umeme Makao Makuu ya Wilaya za Namtumbo, Nyang'hwale na Nkasi; kupatikana Mkandarasi wa kupeleka umeme makao makuu ya

wilaya za Bukombe na Mbogwe; kusainiwa kwa mikataba 35 kati ya Serikali na wakandarasi 16 wa kutekeleza Awamu ya Pili ya Mpango Kabambe wa Usambazaji Umeme Vijijini; kukamilisha ujenzi wa kilomita 24.78 kati ya 47.53 za njia za usambazaji umeme na kufunga transfoma 7 kati ya 24 mkoani Mtwara na kuunganisha umeme kwa wateja 277; na kukamilisha ujenzi wa jumla ya kilomita 11.28 kati ya 28.20 za njia ya umeme ya msongo wa kV 33 na kV 11 katika mkoa wa Lindi. Aidha, ujenzi wa kilomita 59.5 kati ya 72.3 za njia ya umeme ya msongo wa kV 0.4 mkoani Lindi umekamilika na transfoma 5 kati ya 25 zimefungwa.

16. **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa **kilimo** mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na:- kutoa mafunzo ya kuendesha skimu za umwagiliaji kwa maofisa ugani 95 kati ya maafisa 480 waliolengwa, na wakulima 495 waliopata mafunzo hayo ikilinganishwa na lengo la kutoa mafunzo kwa wakulima 195; kupata hati miliki za mashamba makubwa matatu (Bagamoyo - hekta 22,000, Lukulilo hekta 5,526 na Mkulazi - hekta 63,000); kutoa hati za kimila kwa kwa wakulima 1934; kuendelea na ujenzi wa miradi ya umwagiliaji katika ukanda wa SAGCOT katika miradi ya Itete ambapo ujenzi wa ofisi ya mradi umekamilika, na ujenzi wa banio umefikia asilimia 60; usanifu wa banio la Sonjo umekamilika na lile la Lupiro usanifu umefikia asilimia 80. Aidha, ghala la kuhifadhi tani 5,000 za chakula

Songea limekamilika; maghala 26 wilayani Mbozi na manne (4) wilayani Momba yamekarabatiwa kwa asilimia 95. Vilevile, maghala 52 yamefanyiwa tathmini tayari kwa kukarabatiwa.

17. **Mheshimiwa Spika,** katika sekta ya **viwanda,** mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na: kukamilika kwa uchorongaji katika mradi wa makaa ya mawe Mchuchuma na mradi wa chuma Liganga ambao umebaini uwepo wa mashapo ya makaa ya mawe kiasi cha tani milioni 370 na chuma kiasi cha tani milioni 219; kukamilika kwa upembuzi yakinifu na michoro kwa ajili ya ujenzi wa migodi na kiwanda cha chuma; kuendelea na ulipaji fidia kwa eneo la Bagamoyo SEZ ambapo shilingi bilioni 3 zililipwa na hivyo jumla ya fidia iliyolipwa katika eneo hilo imefikia shilingi bilioni 19.9; Tanga SEZ shilingi bilioni 3; na Kituo cha Biashara na Huduma Kurasini shilingi bilioni 20 na hivyo jumla ya fidia iliyolipwa katika eneo hilo imefikia shilingi bilioni 45, kwa kaya 472. Kazi nyingine zilizofanyika ni pamoja na kukamilisha ufungaji wa mitambo na ujenzi wa barabara za ndani katika kiwanda cha kutengeneza viuadudu – Kibaha na kuendelea na kazi ya kubaini teknolojia bora ya uchimbaji wa magadi soda katika bonde la Engaruka.

18. **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa **rasilimali watu,** hadi Juni, 2014, wataalam wapatao 374 waliendelea kugharamiwa masomo na Serikali katika

nyanja maalum zikiwemo mafuta na gesi, urani na madini. Kati ya hao, wanafunzi 76 wanasoma masomo katika fani ya mafuta na gesi katika ngazi za stashahada, shahada na shahada ya uzamili katika vyuo mbalimbali ndani na nje ya nchi. Vilevile, Serikali imeendelea kutekeleza miradi ya ujenzi na ukarabati wa miundombnu ya elimu katika vyuo vikuu, vyuo vya ualimu, ufundi na ustawi wa jamii.

19. **Mheshimiwa Spika,** katika eneo la **huduma za fedha**, mafanikio yaliyopatikana hadi Juni 2014, ni pamoja na: kukamilisha uundwaji wa Benki ya Maendeleo ya Kilimo na kuanza kazi ikiwa ni pamoja na kuiongezea mtaji kufikia shilingi bilioni 90; kuipatia mtaji wa shilingi bilioni 10 Benki ya Rasilimali Tanzania - TIB na hivyo kufikisha mtaji wa shilingi bilioni 152 na benki imeendelea kutoa mikopo kwa sekta mbalimbali zikiwemo kilimo, utalii, na biashara. Vilevile, hadi Juni 2014, Benki ya Maendeleo ya Wanawake iliongezewa mtaji wa shilingi milioni 450 na Serikali.

20. **Mheshimiwa Spika**, pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo, kulikuwa na changamoto mbalimbali zilizojitokeza. Changamoto hizo ni pamoja na:- miradi mingi ipo nyuma ya ratiba kutokana na changamoto mbalimbali ikiwemo upatikanaji wa fedha na madeni ya miaka iliyopita; ugumu wa kupata taarifa za ushiriki wa

sekta binafsi katika uwekezaji unaozingatia vipaumbele vya Mpango wa maendeleo wa mwaka; upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kujirudiarudia kwa baadhi ya miradi kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo kupitwa na wakati na masharti ya wafadhili; na upatikanaji wa ardhi iliyopimwa kwa ajili ya kuwezesha mradi kutekelezwa.

21. **Mheshimiwa Spika**, Serikali imekuwa ikichukua hatua mbalimbali katika kukabiliana na changamoto zilizojitokeza. Hatua hizi ni pamoja na hizi zifuatazo:- kuendelea na juhudi za kuboresha ukusanyaji wa mapato ya ndani (ya kodi na yasiyo ya kodi); uchambuzi wa misamaha ya kodi na kupanua wigo wa kodi; kuanzisha mfuko wa kuwezesha ubia baina ya sekta ya umma na binafsi ili kuongeza ushiriki wa sekta binafsi katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo; na Utekelezaji wa mpango wa matumizi bora ya ardhi ikiwa ni pamoja na kutenga maeneo ya uwekezaji.

22. **Mheshimiwa Spika,** maelezo ya kina kuhusu utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2013/14 na robo ya kwanza kwa mwaka 2014/15 kwa baadhi ya miradi yakijumuisha mafanikio yaliyopatikana kwa upande wa sekta binafsi yapo katika kitabu cha Mapendekezo ya Mpango 2015/16 (Sura ya pili).

## MAENEO MUHIMU YA MAPENDEKEZO YA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA 2015/16

23. **Mheshimiwa Spika,** Mwaka 2015/16, ni wa mwisho katika utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2011/12 – 2015/16), na ni mwaka wa mwisho wa kutekeleza ilani ya uchaguzi ya CCM (2010 – 2015). Hivyo, masuala muhimu yatakayozingatiwa ni pamoja na maandalizi ya mpango wa pili wa maendeleo wa miaka mitano (2016/17 – 2020/21); kufanya uchaguzi mkuu, na kukamilisha miradi inayotekelezwa katika sekta mbalimbali. Serikali itaendelea kutoa kipaumbele katika kuchochea uwekezaji wa sekta binafsi, na hivyo kuongeza ajira na uzalishaji hususan katika sekta ya kilimo kwa lengo la kuendelea kudhibiti mfumuko wa bei na kuimarisha ushindani wa kiuchumi na kuongeza mauzo nje ya nchi.

24. **Mheshimiwa Spika,** shabaha na malengo yaliyowekwa kwa uchumi jumla kwa kipindi cha 2014/15 - 2016/17 ni kama ifuatavyo:-

i. Kuongeza kasi ya ukuaji wa Pato halisi la Taifa kufikia asilimia 7.2 mwaka 2014, asilimia 7.4 mwaka 2015 na asilimia 7.8 mwaka 2016;
ii. Kuendelea kudhibiti kasi ya mfumuko wa bei na kuhakikisha kuwa unabaki kwenye wigo wa tarakimu moja katika kipindi cha muda wa kati;

iii. Kuwa na akiba ya fedha za kigeni kwa kiwango cha kukidhi mahitaji ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa kipindi kisichopungua miezi minne;
iv. Kupunguza kasi ya ukuaji wa ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3) kufikia asilimia 15.5 mwaka 2014/15;
v. Kuongeza ukusanyaji wa mapato ya ndani kutoka asilimia 18.4 ya Pato la Taifa mwaka 2013/14 kufikia asilimia 19.1 ya Pato la Taifa mwaka 2015/16, asilimia 19.8 ya Pato la Taifa mwaka 2017/18;
vi. Kuongeza mikopo kwa sekta binafsi kufikia asilimia 18.8 ya Pato la Taifa Juni, 2015;
vii. Kuongeza tija katika kilimo hususan mazao yenye thamani kubwa ili kuongeza kipato cha mwananchi; na
viii. Kujenga uwezo wa kuhimili changamoto zinazotokana na mabadiliko ya tabianchi.

25. **Mheshimiwa Spika,** Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2015/16 utaandaliwa na kutekelezwa kwa kuzingatia misingi ifuatayo:-

i. Kuendelea kudumisha amani na utawala bora kwa kuwa ni msingi muhimu wa kuwezesha uzalishaji mali, uwekezaji, ukuaji wa uchumi na maendeleo ya kiuchumi na kijamii;
ii. Kuendelea kuimarisha utengamavu wa viashiria vya uchumi jumla na maendeleo ya jamii

ikiwemo ukuaji wa Pato la Taifa, ukusanyaji wa mapato, na mfumuko wa bei;

iii. Kuendelea kusimamia na kuhakikisha uhimilivu wa deni la Taifa;
iv. Kuimarisha utekelezaji wa Sera za Fedha na Bajeti;
v. Kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji;
vi. Kuendelea kuimarika kwa uchumi wa Dunia;
vii. Kuwepo kwa hali ya hewa nzuri; na
viii. Utengamavu wa bei ya mafuta katika soko la dunia.

**Maeneo ya Kipaumbele 2015/16**

26. **Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia masuala muhimu niliyoainisha hapo juu, sasa naomba nielezee kwa kifupi kuhusu vipaumbele katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2015/16.

27. **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa **Miundombinu** maeneo yatakayopewa kipaumbele ni:

i. **Reli:** kutafuta mwekezaji wa kujenga upya reli ya kati kwa kiwango cha kimataifa cha standard gauge (mm 1435); kuboresha miundombinu ya reli ya TAZARA; kuendelea kukamilisha upembuzi wa kina na kumpata mwekezaji wa kujenga reli mpya ya Mtwara – Mbamba Bay; kukamilisha upembuzi wa kina na kumpata Mwekezaji wa Tanga – Arusha – Musoma; na kuendelea

kuboresha usafiri wa reli jijini Dar es Salaam.

ii. **Bandari**: kuendelea kuboresha miundombinu ya bandari hususan miradi iliyoibuliwa katika Programu ya Matokeo Makubwa Sasa; kuendelea kuboresha miundombinu na ununuzi wa vifaa mbalimbali vya kuhudumia shehena katika bandari za Dar es Salaam, Tanga, Mtwara, Kasanga na Kigoma na kukamilisha maandalizi ya ujenzi wa bandari mpya za Mwambani (Tanga), Mbegani (Bagamoyo) na Bandari Kavu ya Kisarawe.

iii. **Nishati**: kuendelea kutekeleza miradi iliyoibuliwa chini ya programu ya Matokeo Makubwa Sasa; kukamilisha ujenzi wa bomba la Gesi kutoka Mtwara na Lindi hadi Dar es Salaam; kuendelea kuboresha miundombinu ya ufuaji, usafirishaji na usambazaji wa umeme mijini na vijijini; kuendeleza uwekezaji katika vyanzo vya nishati mbadala ambavyo ni jadidifu na makaa ya mawe; na kuweka mazingira wezeshi ili Taifa liweze kunufaika na rasilimali ya gesi asilia.

iv. **Barabara:** kutekeleza miradi ya barabara iliyoibuliwa chini ya programu ya Matokeo Makubwa Sasa na ujenzi na ukarabati wa barabara zinazofungua maeneo yenye fursa kubwa kiuchumi, hususan barabara ya Itoni - Mkiu – Ludewa – Manda na michepuko ya Mchuchuma na Liganga.

v. **Usafiri wa Anga:** kuendelea kuboresha miundombinu ya usafiri wa anga ili kuongeza ufanisi; na kuendelea na kazi ya ujenzi na ukarabati wa viwanja vya ndege katika maeneo ya kimkakati, ikiwa pamoja na jengo jipya la abiria katika kiwanja cha Julius Nyerere *(Terminal III).*

vi. **Maji Safi na Majitaka:** kuendelea na utekelezaji wa miradi ya maji chini ya progamu ya Matokeo Makubwa Sasa na kuimarisha upatikanaji huduma za maji safi na majitaka katika Jiji la Dar-es Salaam na miji mingine nchini kwa kuboresha, kukarabati na kuongeza miundombinu na vyanzo vipya; kuimarisha na kuongeza miundombinu ya maji vijijini ili kuweza kuwafikia wananchi wengi zaidi.

vii. **Teknolojia ya Habari na Mawasiliano:** kuendelea na ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano; kuanzisha maeneo maalum ya TEHAMA; utekelezaji wa mradi wa Anuani za Makazi na Misimbo ya Posta; na kuendeleza Mradi wa Serikali mtandao.

28. **Mheshimiwa Spika,** katika sekta ya **Kilimo,** maeneo yatakayopewa kipaumbele ni:- kuendelea na utekelezaji wa miradi ya kilimo chini ya programu ya Matokeo Makubwa Sasa; kuendeleza miradi ya

umwagiliaji hususan katika ukanda wa SAGCOT; na ujenzi wa maghala ya kuhifadhia chakula.

29. **Mheshimiwa Spika,** katika sekta ndogo ya **Mifugo na Uvuvi**, maeneo ya kipaumbele ni: kuboresha miundombinu ya mifugo kama vile malisho, majosho, na malambo; kuongeza thamani ya mazao ya mifugo na uvuvi; kukamilisha upembuzi yakinifu kwa ajili ya ujenzi wa bandari ya uvuvi; kujenga na kuimarisha vituo vya uhamilishaji na kukuza huduma na miundombinu ya uzalishaji wa samaki.

30. **Mheshimiwa Spika,** katika sekta ya **Viwanda,** maeneo ya kipaumbele ni: kuendelea kutambua na kutenga maeneo ya ardhi ya uwekezaji, kukamilisha malipo ya fidia na kujenga barabara kutoka Zinga hadi Kondo kwa ajili ya kuingilia eneo maalum la uwekezaji *(SEZ)* Bagamoyo; ujenzi wa kituo cha Biashara na Huduma Kurasini; kuongeza kasi ya kuvutia wawekezaji na kujenga mazingira wezeshi katika sekta ya viwanda; kuanza ujenzi wa mgodi wa makaa ya mawe – Mchuchuma; na chuma – Liganga; na kufanya usanifu kwa ajili ya ujenzi wa kiwanda cha chuma; kulipa fidia kwa wakazi wa kijiji cha Engaruka (takriban kaya 30 mpaka 40) na ujenzi wa miundombinu ya maji safi kutoka Selela mpaka Engaruka (km 30) kwa ajili ya matumizi ya kiwanda na wananchi; na kutafuta wabia kwa ajili ya kuendeleza mradi wa magadi soda - Engaruka; kuimarisha Mfuko wa Maendeleo kwa

Wajasiriamali ili kuwezesha utoaji wa mikopo kwa wakulima wadogo kununua mashine za kusindika mazao na kuwapatia mafunzo mbalimbali; na uhaulishaji wa teknolojia ya uzalishaji wa matrekta na zana za kilimo - Nyumbu.

31. **Mheshimiwa Spika,** katika eneo la **Maendeleo ya Rasilimali Watu,** maeneo ya kipaumbele ni: kuendelea na utekelezaji wa miradi ya elimu chini ya programu ya Matokeo Makubwa Sasa; kuongeza idadi ya wataalam katika sekta za afya, elimu na kilimo; kuendelea kutoa mafunzo katika nyanja maalum hususan katika gesi na mafuta, chuma, urani, na TEHAMA; kuanzisha Chuo Kikuu cha Kilimo cha Mwalimu Nyerere, Butiama; na kuendeleza elimu ya ufundi stadi kwa kuongeza na kuboresha miundombinu na mitaala katika vyuo vikuu, vyuo vya ualimu, ufundi na maendeleo ya jamii.

32. **Mheshimiwa Spika,** katika sekta ya **Huduma za Utalii, Biashara na Fedha**, maeneo ya kipaumbele ni: kuongeza mitaji na matawi katika Benki ya Kilimo, Benki ya Rasilimali na Benki ya Wanawake; kujenga uwezo wa utoaji huduma na mikopo; na mafunzo kwa wajasiriamali. Vilevile, Serikali itaendelea kushirikisha sekta binafsi kuwekeza zaidi katika maeneo yenye vivutio vya utalii, na kuendelea kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji nchini ili kuongeza kasi ya uwekezaji katika utalii, huduma za

kibenki na biashara.

33. **Mheshimiwa Spika,** maelezo ya kina kuhusu maeneo ya vipaumbele kwa mwaka 2015/16 yapo katika Kitabu cha Mapendekezo ya Mpango wa Taifa wa Maendeleo 2015/16 (Sura ya tatu).

## UGHARAMIAJI WA MPANGO WA MAENDELEO 2015/16

34. **Mheshimiwa Spika,** Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2015/16 utagharamiwa na vyanzo mbalimbali vya mapato ikiwa ni pamoja na mapato ya ndani, misaada pamoja na ushiriki wa sekta binafsi. Serikali itaendelea kukopa ndani na nje ya nchi hususan mikopo yenye masharti nafuu kwa kuzingatia ukomo wa uhimilivu wa deni la Taifa, ili kufanikisha utekelezaji wa miradi. Katika bajeti ya maendeleo 2015/16 Serikali inakusudia kutenga kiasi cha Tshs. bilioni 5,777 ili kutekeleza miradi ya maendeleo ambapo fedha za ndani ni shilingi bilioni 3,277 na fedha za nje shilingi bilioni 2,500.

35. **Mheshimiwa Spika,** Serikali itaendelea kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji nchini, ili kuwezesha sekta binafsi kuchangia katika kufanikisha utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kipaumbele itakuwa ni kutumia rasilimali chache kuchochea uwekezaji wa sekta binafsi pamoja na kuendelea kuboresha mazingira ya kibiashara na uwekezaji ili kuvutia uwekezaji katika maeneo ya kipaumbele na yenye kuleta matokeo makubwa.

## MAJUKUMU YA UTEKELEZAJI

36. **Mheshimiwa Spika,** mara baada ya Mapendekezo haya kuridhiwa na Bunge, Wizara, Idara zinazojitegemea na Wakala za Serikali zitatakiwa kuandaa na kuwasilisha Tume ya Mipango miradi itakayotekelezwa katika sekta zao kwa mwaka 2015/16. Serikali itafanya uchambuzi na miradi itakayopitishwa itajumuishwa katika kitabu cha Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2015/16 na kitabu cha Bajeti ya Maendeleo 2015/16 (Vol 4). Aidha, Mamlaka za Serikali za Mitaa zitatakiwa kuainisha miradi ya maendeleo na kuwasilisha mapendekezo ya miradi hiyo Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI na Wizara ya Fedha kwa ajili ya kujumuisha katika kitabu cha Bajeti ya Maendeleo (Vol 4).

## HITIMISHO

37. **Mheshimiwa Spika**, naomba Kamati yako ijadili na kuishauri Serikali, hususan katika maeneo ya kipaumbele yanayotarajiwa kutekelezwa mwaka 2015/16.

38. **Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja.